

TANGAZO LA SERIKALI NA.....LA TAREHE.....

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA MIJI)

(SURA YA 288)

## SHERIA NDOGO

*(Zimetungwa chini ya kifungu cha 89)*

### SHERIA NDOGO ZA (USAFI WA MAZINGIRA) ZA HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILALA ZA MWAKA 2015

<b>Jina</b>	1.	Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria ndogo za (Usafi wa Mazingira) za Halmashauri ya Manispaa ya Ilala za Mwaka 2015
<b>Matumizi</b>	2	Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lolote chini ya Mamlaka ya Halmashauri ya Manispaa ya Ilala na zitaanza kutumika mara baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.
Tafsiri.	3	<p>Katika Sheria ndogo hizi isipokuwa itakapoelezwa vinginevyo-</p> <p>“Ada” maana yake ni malipo yanayotakiwa kufanywa na kampuni, viwanda, mtu binafsi, taasisi kwa ajili ya kupima Afya au kufanyiwa uchunguzi wa kiafya kwa mfanyabiashara wa chakula, au vinyozi, wasusi wa nywele na wafanyakazi wa nyumba za kulala wageni, mhudumu wa biashara ya chakula au mfanyakazi wa kiwandani ndani ya Halmashauri ya Manispaa ya Ilala;</p> <p>“Adha” maana yake hali yoyote mbaya yenye kuleta madhara juu ya afya ya watu kwa ujumla;</p> <p>“Afya” maana yake hali timilifu ya kimwili, kiakili na kijamii na wala sio tu kutokuwa na ugonjwa au kilema;</p> <p>“ Afisa mwidhiniwa” maana yake Afisa yeyote aliyeteuliwa kusimamia utekelezaji wa sheria ndogo hizi;</p> <p>“Bafu” maana yake chumba maalum kilichojengwa kwa madhumuni ya kuogea.</p> <p>“Chakula” maana yake kitu chohcote kinacholiwa na</p>

		<p>binadamu na inajumuisha maji na dawa;</p> <p>“Choo bora” maana yake choo cha lindi chenye shimo lililojengwa madhubuti au choo chochote cha maji chenye sakafu imara, banda imara la kudumu, imezekwa, kina mlango imara kama cha lindi kimeongezwa bomba la kutoa hewa chafu na chenye mfuniko kwenye tundu la choo;</p> <p>“Chukizo la Afya” maana yake kitu chochote kinachoweza kuleta kinyaa machoni kwa kuona, kunusa, hewa chafu, madhara au kuhatarisha Afya za binadamu na wanyama;</p> <p>“Halmashauri” maana yake Halmashauri ya Manispaa ya Ilala;</p> <p>“Jengo la Biashara” maana yake jengo lolote lililojengwa na kuidhinishwa na mamlaka kufanya biashara iliyokusudiwa;</p> <p>“Kaya” maana yake mtu mzima anayejitegemea mwanamke au mwanaume, na mtoto au watoto inayoishi aidha kwenye nyumba nzima au ndani ya chumba kimoja kwenye maeneo ya Kata za Halmashauri;</p> <p>“kikundi cha usafishaji” maana yake kikundi chochote cha watu kinachosajiliwa kufanya shughuli za usafi wa mazingira na hasa za udhibiti wa uharibifu wa mazingira katika maeneo ya Halmashauri;</p> <p>“kituo cha maji machafu” maana yake sehemu maalum iliyotengenezwa kwa ajili ya ukaguzi wa mfereji ambacho kina mfuniko usioruhusu hewa kutoka.</p> <p>“kituo cha taka” maana yake kizimba cha taka au chombo maalum cha kuhifadhia taka, kasha ”refuse bin container” ambayo imewekwa na Halmashauri kwa madhumuni ya Jamii inayoishi jirani kuweka taka ngumu kabla ya kusafirishwa hadi kwenye jalala la taka ngumu la Halmashauri;</p> <p>“kutupa taka ngumu” maana yake kukusanya taka zote zinazozalishwa na kaya, kampuni, sehemu ya biashara, ofisi, taasisi, ofisi ya serikali n.k na kuzipeleka hadi kwenye jalala la Halmashauri, jalala kuu kwa madhumuni ya kuzitupa ndani ya jalala kwa mujibu wa kanuni zilizowekwa na Halmashauri;</p>
--	--	--

	<p>“Mabwawa ya maji taka” maana yake mabwawa yaliyojengwa kwa madhumuni ya kuhifadhi na kutakasa maji taka yanayotokana na kuosha vyombo, kutoka vyooni, kutoka bafuni, kufua nguo, kuosha nywele au shughuli zozote za nyumbani na viwanda;</p> <p>“Magonjwa ya mlipuko” maana yake ni magonjwa yanayotokea kwa muda mfupi ya kuambukiza na kuenea kwa haraka na kuathili watu wengi ndani ya muda mfupi yanayoweza kutolewa amri ya taadhari, kupooza, kipindupindu, kuhara, louse bare typhus, (relapsing) fever, surua na homa ya matumbo;</p> <p>“Mazalio ya wadudu” maana yake sehemu ambayo wadudu hufanya mazalio au kuishi kwa minajiri ya kufanya mzunguko wa maisha na baadae huleta maadhara kwa binadamu.</p> <p>“Mifugo” maana yake ng’ombe, punda, nguruwe, mbuzi, kondoo au kuku na wanyama wengine wote wafugwao majumbani;</p> <p>“Mkurugenzi” maana yake Mkurugenzi wa Halmshauri au Afisa yeyote atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;</p> <p>“Mzalishaji wa taka ngumu” maana yake mtu yeyote, kaya taasisi, biashara au kiwanda ambaye katika kutekeleza shughuli zake za kila siku huzalisha taka ngumu na ofisi za serikali.</p> <p>“Mtandao wa maji taka” maana yake mfumo wa bomba kuu lililojengwa kwa madhumuni ya kupokea na kusafirisha taka miminika toka kwenye mifereji ya maji na kuyapeleka kwenye mabwawa ya maji taka au baharini.</p> <p>“Mzalishaji wa maji taka” maana yake mtu, shirika, kiwanda au taasisi ambapo shughuli zake kwa namna yoyote ile huzalisha maji taka;</p> <p>“Pipa la taka” maana yake chombo chochote kilichokubaliwa na Halmashauri kitumike kama chombo cha kuhifadhi taka ngumu zinazozalishwa majumbani, sehemu za biashara, maofisini, pamoja na chombo maalum kinachobebwa na gari la takataka;</p>
--	--

	<p>“Taka ngumu” maana yake kitu chochote ambacho baada ya kukitumia hakina thamani yoyote kwa jamii inayohusika, uwepo wake katika eneo husika unaweza kusababisha machukizo ya kiafya na kuhatarisha afya ya jamii.</p> <p>“Taka za majumbani” maana yake mabaki ya vyakula, maganda ya matunda, majivu, marapurapu ya nguo, karatasi za aina mbalimbali, kinyesi cha mifugo, taka za bustani na vitu vingine ambavyo baada ya kuvitumia hutupwa;</p> <p>“Taka ndogo ndogo” maana yake mabaki ya vocha za simu, chupa za maji, chupa za juisi, maganda ya pipi, chocolate, ice cream, pakiti za sigara, vichungi vya sigara, vizibo vya chupa, maganda ya matunda, miwa, mahindi, machungwa, mananasi, masalia ya magunzi, mbogamboga, magazeti na karatasi za aina mbalimbali, na vitu vingine ambavyo baada ya kuvitumia hutupwa;</p> <p>“Taka za biashara” maana yake ni aina yoyote ya taka ambazo hupatikana au hutokana na shughuli mbalimbali za kibiashara;</p> <p>“Taka za viwanda” maana yake aina yoyote ya taka ambazo hutokana na uzalishaji wa shughuli mbalimbali viwandani;</p> <p>“ Taka hatari” maana yake aina yoyote ya taka ambayo kwa njia fulani hubaki kwenye mazingira na hatima yake ni kusababisha madhara kwa afya ya jamii ikiwa ni pamoja na taka zitokanazo na shughuli za hospitali, shughuli za mionzi “X –ray, films, radio active materials”, vitu vyenye ncha kali kama sindano, chupa au taka zitokanazo na shughuli za uzalishaji viwandani kama vile (dry batteries), mercury, madawa mbalimbali, mabaki ya vyuma, kemikali, gesi mbalimbali;</p> <p>“Taka miminika” maana yake maji yaliyokwisha tumika au chafuliwa kwa namna yoyote ile ambayo yanajumuisha maji machafu toka chooni, bafuni, jikoni, viwandani, maji yaoshewayo vyombo, maji yaliyofuliwa nguo, kuosha nywele, kuosha vyakula na yaliyopigiwa deki;</p> <p>“Ufugaji wa afya” maana yake ufugaji ndani ya eneo lililoruhusiwa na si nje ya banda au jingo.</p> <p>“ Uchunguzi wa afya” maana yake ni hali ya mtu kupima afya</p>
--	---

		<p>yake kwa kuchukuliwa vipimo vya ndani na nje ya mwili ili kubaini kuwepo kwa vijidudu vya Magonjwa vinavyoweza kuleta maambukizi;</p> <p>“Ugonjwa wa kuambukizwa” maana yake ugonjwa wowote uambukizwao toka kwa mtu na mtu au mtu kwa mnyama, mtu kwa mdudu mfano kifua kikuu, brucellosis, kimeta, safura, surua, kipindupindu au uti wa mgongo n.k.</p>
<b>Utupaji wa Takataka.</b>	<p>4 . (1)</p> <p>(2)</p> <p>(3)</p> <p>(4)</p> <p>(5)</p>	<p>Ni marufuku kutupa takataka au uchafu wowote au kuacha kuwepo takataka au uchafu kwenye nyumba, biashara, kiwanja, mfereji wa maji ya mvua, barabara au mahali popote pasipotengwa kwa shughuli hiyo.</p> <p>Ni wajibu wa kila mmiliki wa nyumba iliyoko ndani ya Halmashauri kuhakikisha kwamba:-</p> <p>(a) Ana pipa lenye mfuniko litakalotumika kutupia taka ngumu; na</p> <p>(b) Anasafisha mfereji wa maji ya mvua uliopita karibu na nyumba yake mfereji na maeneo yanayozunguka nyumba yake yanakuwa safi muda wote;</p> <p>Gari lolote lilobeba taka ngumu linatakiwa liwe limefunikwa kiasi cha kuzuia taka ngumu zisionekane wala kumwagika chini na kuleta adha kwa watu na uchafuzi wa mazingira kwa ujumla.</p> <p>Ni wajibu kila mmiliki wa daladala anapaswa kuweka chombo cha kuhifadhia takatata kwenye gari.</p> <p>Abiria au mwenye gari yeyote haruhusiwi kutupa takataka ovyo barabarani.</p>

<p><b>Ada ya uzoaji Taka.</b></p>	<p>5 - (1)</p> <p>(2)</p>	<p>Ni wajibu wa kila kaya, taasisi mbalimbali na wizara kuhakikisha kwamba inalipa ada ya uzoaji taka kwa viwango vilivyoainishwa kwenye jedwali la kwanza la Sheria ndogo hizi ikiwa ni gharama ya kusafirisha taka ngumu kutoka kwenye nyumba yake hadi sehemu iliyotengwa maalum kwa ajili kuzoa taka ngumu.</p> <p>Halmashauri inaweza kumteua mtu yeyote, kikundi cha watu, kampuni au taasisi kukusanya ada ya uzoaji taka kwa niaba yake.</p>
<p><b>Matumizi ya vyoo bora.</b></p>	<p>7 (1)</p> <p>(2)</p> <p>(3)</p>	<p>Kila mmiliki nyumba katika eneo la Halmashauri anatakiwa kuwa na choo bora na safi kwa matumizi ya wakazi wa nyumba hiyo.</p> <p>Kila mmiliki wa nyumba inayotumika katika shughuli ya ibada, biashara, hoteli, mgahawa, nyumba ya kulala wageni, baa, klabu, gereji au shughuli yoyote inayokusanya watu wengi kwa pamoja anatakiwa kuweka na kutunza vyoo vya kutosha kwa jinsia za kiume na kike.</p> <p>Iwapo Halmashauri itagundua kuwa nyumba yoyote haina choo au choo kilichopo hakifai kwa matumizi ya binadamu, Halmshauri itakuwa na uwezo wa kuchukua hatua yoyote inayoona inafaa ikiwa ni pamoja na kuzuia nyumba hiyo isitumike hadi choo kitakapojengwa au kurekebishwa.</p>
<p><b>Udhibiti wa mazalio ya wadudu.</b></p>	<p>8.</p>	<p>Kila mwenye nyumba au mpangaji anawajibika kuhakikisha kuwa hakuna mazalia ya wadudu kama vile mbu kwenye nyumba yake au karibu na nyumba yake kwa kuondoa maji yaliyokusanyika, kufyeka majani au kuharibu kitu chochote kinachoweza kuwa mazalio ya wadudu au panya.</p>
<p><b>Udhibiti wa Biashara</b></p>	<p>9 .</p>	<p>Ni marufuku kwa mtu yeyote kufanya biashara ya aina yoyote kwenye maeneo ambayo hayajatengwa rasmi kwa shughuli za biashara.</p>
<p><b>Udhibiti wa uuzaji wa vyakula.</b></p>	<p>10 . (1)</p> <p>(2)</p>	<p>Ni marufuku kwa mtu yeyote kuuza vyakula kwenye eneo lolote la Halmashauri bila kibali cha maandishi cha Halmashauri.</p> <p>Mtu yeyote anayetaka kufanya biashara ya kuuza chakula atatuma maombi kwa Halmahauri na iwapo Halmashauri</p>

	(3)	itaridhika na maombi yake atapatiwa kibali.
	(4)	Halmashauri inaweza kufuta kibali kilichotolewa kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (2) iwapo mtu aliyepewa kibali atakiuka masharti ya kibali hicho.
		Kila mmiliki wa kiwanda ni lazima awe na eneo la kantini kwa wafanyakazi wake.
<b>Ukataji wa miti.</b>	12. (1)	Ni marufuku kwa mtu yeyote au kampuni au shirika kukata au kuharibu mti wa aina yoyote ndani ya Halmashauri bila kibali cha Halmashauri.
	(2)	Mtu yeyote atakayekata na kuharibu mti wowote atawajibika kulipa gharama za kupanda na kukuza mti mwingine.
<b>Kujisaidia.</b>	13.	Ni marufuku kwa mtu yeyeto kujisaidia haja ndogo na haja kubwa ovyo katika eneo ambalo siyo choo.
<b>Wajibu wa kupima afya.</b>	14.	Kila mmiliki wa hoteli, migahawa, baa za aina zote za kigeni au kienyeji, bucha, sehemu za kuokea mikate, nyumba za kulala wageni, salooni, glosari au eneo lolote linaloshughulika na vyakula vilivyotengenezwa kwa ajili ya kuuza atawajibika kuhakikisha kuwa wahudumu wake wamepimwa afya zao kabla ya kuanza kazi na atahakikisha kuwa wanapimwa afya zao kila baada ya miezi sita.
<b>Wajibu wa kutunza vyanzo vya maji.</b>	15 (1)	Ni marufuku kwa mtu yeyote:-  (a) Kunawa, kuoga au kufulia nguo au kunywesha mifugo karibu au kwenye chanzo cha maji kama vile chemchem, kisima au chanzo kingine chochote cha maji, au kunywesha mifugo kwenye chanzo cha maji kinachotumika kwa matumizi ya nyumbani ili kwenye sehemu iliyotengwa kwa shughuli hizo;  (b) Kujenga boma la mifugo karibu au kuruhusu mkojo au maji machafu kuelekea kwenye au karibu na chanzo cha maji kwa matumizi ya binadamu.  (c) Kufuga mifugo ya aina yoyote bila kibali cha Halmashauri; au

		<p>(d) Kuacha mifugo au kusababisha mifugo kuzurura ovyo mitaani; barabarani au kuchungwa kwenye eneo lolote lisiloruhusiwa,</p> <p>(2) Mfugo wowote utakaokutwa ukizurura au kuchungwa kwenye eneo lisiloruhusiwa utamakakwa na Halmashauri na mwenye mifugo atalazimika kulipa faini isiyoziidi shilingi elfu hamsini na gharama za kukamata na kutunza mifugo na kiasi chohcote kinachobakia atarudishiwa mwenye mifugo.</p> <p>(3) Mfugo wowote utakaoshindwa kukombolewa ndani ya muda wa siku saba utauzwa kwa njia yam nada ili kulipia faini, gharama za ukamataji na utunzaji wa mfugo na kiasi chochote kitakachobaki atarudishiwa mwenye mifugo.</p>
<b>Udhibiti wa maegesho</b>	16.	<p>Ni marufuku kwa mtu yeyote:-</p> <p>(a) Kuegesha gari eneo ambalo linazuia usafi kufanyika au kuzuia magari au watu kupita.</p> <p>(b) Ni marufuku kuegesha gari bovu barabarani au maeneo yasiyoruhusiwa.</p> <p>(c) Kuosha gari kwenye eneo ambalo halijatengwa rasmi kwa kazi hiyo: au</p> <p>(d) Ni marufuku kwa mtu yeyote kuruhusu gari kuoshwa katika sehemu isiyoruhusiwa.</p> <p>(e) Kupanga bidhaa kwenye njia ya wapitao kwa miguu, uchochoro, kwenye pavement.</p> <p>(f) Kila mwenye jengo katikati ya mji ajenge pavement mbele ya jengo lake.</p>
<b>Udhibiti wa ubebaji kokoto, mawe na mchanga.</b>	17. (1)	Mtu yeyote atakayesafirisha mawe, mchanga au kokoto katika eneo la Halmashauri atahakikisha kuwa chombo anachotumia kusafirisha mchanga, mawe au kokoto kimefunikwa ili kuzuia mchanga, kokoto au mawe kumwagika au kuchafua mazingira.
<b>Uteuzi wa Wakala.</b>	18.	Halmashauri inaweza kuteua mtu yeyote, kikundi cha watu, Kampuni au taasisi kusimamia utekelezaji wa Sheria ndogo



		hizi.
<b>Kosa.</b>	19.	Mtu yeyote atakayekiuka masharti ya Sheria ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua shilingi elfu hamsini au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili jela au vyote kwa pamoja faini na kifungo.
<b>Kifutwa kwa Tangazo la Serikali na 111/2011</b>	20	Sheria ndogo ya (Usafi wa Mazingira) ya Halmashauri ya Manispaa ya Ilala za Mwaka 2011 zimefutwa.

## **JEDWALI LA KWANZA**

### **Mgawanyo wa Kata kulingana na Kipato**

#### **Kanda “A” - Kipato cha Juu.**

1. Upanga Mashariki
2. Upanga Magharibi
3. Kisutu
4. Mchafukoge
5. Gerezani
6. Kivukoni
7. Kariakoo

#### **Kanda “B” - Kipato cha Kati**

1. Jangwani
2. Ilala
3. Kinyerezi
4. Tabata
5. Kimanga
6. Mchikichini
7. Segerea

#### **Kanda “C” - Kipato cha Chini**

1. Buguruni
2. Kipawa
3. Kiwalani
4. Pugu
5. Gongo la Mboto
6. Majohe
7. Kivule
8. Ukonga
9. Kitunda
10. Chanika
11. Msongola
12. Vingunguti

## JEDWALI LA PILI

### Ada za uzoaji Taka

Na.	Aina ya Makazi	Kipato cha juu	Kipato cha Kati	Kipato cha Chini
1	Nyumba za zamani za chini	5000	5000	5000
2	Nyumba za zamani za ghorofa usanifu wa kawaida (kwa kaya)	15,000	10,000	5,000
3.	Nyumba Mpya za chini	10,000	7,000	5,000
4.	Nyumba Mpya za Ghorofa usanifu wa kawaida	15,000	10,000	5,000
5.	Nyumba Mpya za Ghorofa usanifu wa kisasa	20,000	15,000	10,000
6.	Nyumba ya Pekee (Bungalow)	30,000	25,000	20,000
7.	Nyumba ya Pekee yenye nyumba za huduma (Villa)	50,000	40,000	30,000
8.	Penthouse	50,000	40,000	30,000

NA.	AINA YA MZALISHAJI WA TAKA	KIWANGO CHA ADA/USHURU KWA MWEZI				
		KIPATO CHA JUU		KIPATO CHA KATI		KIPATO CHA CHIN
9	Hostel (kwa mpangaji/mkazi)	500		500		500
10	Hostel (kwa chumba)	2,000		2,000		2,000
11	Nyumba ya kulala wageni	50,000		30,000		30,000

12	<b>OFISI:</b>						
	* Ofisi - 01 - 10 wafanyakazi	50,000		20,000		20,000	
	* Ofisi - 11 - 50 wafanyakazi	100,000		100,000		100,000	
	* Ofisi - 51 - 100 wafanyakazi	200,000		200,000		200,000	
	* Ofisi - 101- zaidi ya wafanyakazi	400,000		300,000		300,000	
	<b>BENKI</b>						
13	Tawi la Benki ya Biashara	500,000		500,000		500,000	
14	Duka la kubadilishia fedha	200,000		200,000		200,000	
15	Ofisi za ATM	100,000		100,000		100,000	
16	Ofisi za Luku	100,000		100,000		100,000	
	<b>VYAKULA NA VINYWAJI</b>						
17	Hoteli na Mgahawa	60,000		30,000		20,000	
18	Sehemu ya kutengenezea chai na vitafunwa (Tea Room (Snacks & soft drinks))	20,000		15,000		10,000	
19	Café (Food, snacks & soft drinks)	30,000		20,000		15,000	
20	Duka la vyakula na vinywaji (Grocery)	20,000		15,000		10,000	
21	Baa (pombe, vinywaji baridi na vitafunwa)	50,000		30,000		20,000	

22	Baa na Mgahawa	75,000		50,000		30,000	
23	Baa na Nyumba ya kulala wageni	75,000		50,000		30,000	
24	Baa, nyumba ya wageni na ukumbi wa starehe	100,000		60,000		40,000	
25	Baa na ukumbi wa starehe	100,000		50,000		30,000	
26	Baa, ukumbi wa starehe na mgahawa	150,000		75,000		50,000	
27	Duka la kuuza "Ice cream"	20,000		10,000		10,000	
28	<b>HOTELI:</b>						
	01 - 10 Vyumba	150,000		100,000		50,000	
	11 - 20 Vyumba	250,000		250,000		250,000	
	21-30 Vyumba	350,000		350,000		350,000	
	31-40 Vyumba	450,000		450,000		450,000	
	41-50 Vyumba	550,000		550,000		550,000	
	51 - 70 Vyumba	650,000		650,000		650,000	
	70-100 Vyumba	750,000		750,000		750,000	
	101 - zaidi	1,500,000		1,500,000		1,500,000	
29	Bucha ya nyama na samaki wabichi	15,000		10,000		5,000	
	<b>DUKA (JUMLA NA REJAREJA)</b>						
30	* Vyakula na bidhaa mchanganyiko	30,000		15,000		10,000	

31	* Nguo	30,000		10,000		5,000
32	* Vifaa vya umeme au Simu (Electronic , Phone , Phone Accesories& electrical appliances)	60,000		40,000		25,000
33	* Vifaa vya ujenzi (Hard ware stores)	60,000		40,000		25,000
28	* Vitabu, shajara na vitu vya zawadi	20,000		10,000		5,000
29	* Sonara na vipodozi (Jewelry & Cosmetics)	20,000		10,000		5,000
30	* Duka la samani (Furniture & Machinery)	50,000		30,000		20,000
31	* Vinywaji na Pombe kali (Beverages and Liquor stores)	30,000		20,000		10,000
32	* Vipuri na vifaa (Spare parts and tools)	50,000		15,000		10,000
33	* Duka la vifaa chakavu (Junk shops)	50,000		20,000		10,000
	<b>KARAKANA NA VIWANDA</b>					
34	* Fundi seremala	30,000		20,000		10,000
35	* Karakana ya chum(Metal W/Shops)	30,000		20,000		10,000
36	* Karakana ya magari (Motor Garages)	50,000		30,000		20,000

37	Sonara na uhunzi wa vito (Jewelry and black smiths)	15,000	10,000	5,000	
38	shughuli za vioo(Glass works)	50,000	30,000	20,000	
39	* Mchapishaji (Printers)	500,000	500,000	500,000	
40	* Machine ya mbao kwa ujazo wa mita 1 (Saw mills per M <sup>3</sup> )	15,000	15,000	15,000	
41	<b>Viwanda vidogo na vikubwa</b>				
	: kwa tani moja ya taka	40,000	40,000	40,000	
	: kwa ujazo wa mita za mraba moja (m <sup>3</sup> )	25,000	25,000	25,000	
42	* Umeme na matengenezo ya elektroniki (Electrical and electronic repairs)	25,000	15,000	10,000	
43	* Magurudumu na matengenezo	20,000	15,000	10,000	
	<b>BIASHARA NDOGO NA SEKTA ISIYO RASMI:</b>				
44	* Fundi cherehani	20,000	10,000	5,000	
45	* Seremala	20,000	10,000	5,000	
46	* fundi viatu (Cobler / Shoer repair)	8,000	4,000	2,000	
47	* Saluni ya nywele	20,000	10,000	5,000	
48	* Dobi and dry cleaner	20,000	10,000	5,000	
49	* Genge kwa meza moja	5,000	3,000	2,000	

50	* Huduma za shajara	20,000		10,000		5,000	
51	* Huduma za "Internet"	10,000		5,000		3,000	
	<b>HUDUMA ZA AFYA (Taka zisizokuwa za hatari)</b>						
52	* Duka la Dawa baridi	50,000		30,000		20,000	
	<ul style="list-style-type: none"> <li>Duka la Dawa La Jumla (Wholesale Pharmacy)</li> <li>Duka la Dawa Rejareja (Retail Pharmacy)</li> </ul>	200,000		200,000		200,000	
		150,000		100,000		50,000	
53	* Maabara ya vipimo	20,000		10,000		5,000	
54	* Zahanati	50,000		30,000		15,000	
55	* Kituo cha Afya	50,000		30,000		15,000	
56	* Madawa asilia	20,000		10,000		5,000	
57	* Hospital	300,000		300,000		300,000	
58	* Kliniki	25,000		15,000		10,000	
59	* Hospitali ya Rufaa	4,000,000		4,000,000		4,000,000	
	<b>TAASISI ZA MAFUNZO</b>						
60	<b>Kituo cha kulelea watoto, Shule za kutwa na Vyuo</b>						
	* 01 - 200 wanafunzi	40,000		30,000		15,000	
	* 101 - 500 wanafunzi	80,000		50,000		30,000	
	* 501 - 1,000 wanafunzi	150,000		100,000		80,000	
	* 1001 - zaidi ya wanafunzi	250,000					



				250,000		250,000	
<b>61</b>	<b>Shule na Chuo kutwa</b>						
	* 01 - 200 -wanafunzi	60,000		60,000		60,000	
	* 101 - 500-wanafunzi	150,000		150,000		150,000	
	* 501 - 1000-wanafunzi	250,000		200,000		150,000	
	* 1001 - zaidi ya wanafunzi	400,000		300,000		300,000	
	<b>VITUO CHA MAFUTA</b>						
62	* kituo kikubwa cha mafuta	100,000		100,000		100,000	
63	* kituo kidogo cha mafuta	60,000		60,000		60,000	
64	* kituo cha mafuta ya Taa	15,000		15,000		15,000	
65	* Kituo cha kuuzia Gasi	15,000		15,000		15,000	
66	* Kibanda cha kuuzia mkaa	100,000		50,000		25,000	
67	Msikiti au Kanisa bila kuwa na shughuli zingine za kibiashara	20,000		10,000		5,000	
68	Msikiti au Kanisa ukiwa na shughuli zingine za kibiashara	50,000		25,000		15,000	
	<b>HUDUMA NYINGINEZO</b>						
69	* Jumba la starehe na klabu	250,000		100,000		50,000	
70	* Ofisi za ulinzi	20,000		10,000		5,000	
71	* Kituo cha Taxi kwa siku	300		250		200	
72	* Kituo cha Basi kwa mwezi	10,000		10,000		10,000	
73	* Kituo cha Daladala	5,000		5,000		5,000	
74	* Lori la mizigo kushusha(Eneo rasmi kwa tripu moja)	15,000		10,000		5,000	
75	* Lori la mizigo kushusha(Eneo ambalo sio rasmi kwa tripu moja)	5,000		5,000		5,000	

76	Duka la Simu, Kampuni ya simu kwa mnara wa mawasiliano (Mobile - Phone Companies/Per booster power (Mnara))	60,000		60,000		60,000	
77	* Kituo cha Transiforma ya Umeme (Electric transformer stations)	100,000		80,000		50,000	
	<b>TAKA ZENYE UJAZO MKUBWA (BULKY AND BUNDLE WASTE)</b>						
78	* Taka za bustani kwa mita mraba moja ( M <sup>3</sup> )	25,000		25,000		25,000	
79	* Taka za viwandani kwa tani	40,000		40,000		40,000	
80	* Taka za masoko kwa tani	40,000		40,000		40,000	
81	* Taka za Biashara kwa tripu (Supermarkets)	500,000		500,000		500,000	
82	* Taka za uvunjaji jengo kwa tani moja (Demolition Debris per ton)	50,000		50,000		50,000	

Nembo na mhuri wa Halmashauri ya Manispaa ya Ilala umebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kwa kufuata Azimio lililopitishwa kwenye mkutano wa Baraza la Madiwani uliofanyika mnamo tarehe 03 mwezi Julai, Mwaka 2015.

.....  
*Isaya Moses Mngurumi,*  
**Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa Ilala**

.....  
*Jerry William Silaa*  
*Mstahiki Meya,*  
**Halmashauri ya Manispaa Ilala**

**NAKUBALI**

.....  
*Mizengo P. Pinda (MB),*  
**WAZIRI MKUU**

**DODOMA**

**.../...../2015**